Toleo 65 - Dhul Qa'adah 1443 AH / Juni 2022 M

UQAB
Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Kupaa Bei ya Mafuta Tanzania: Chanzo Mfumo wa Ubepari

**HABARI NA MAONI**
Sera za Kirasilimali Zinakuza Kiwango cha Uzazi Jumla (TFR) kuwa Chini

**MATOLEO**
Nidhamu ya Uchumi ya Kiislamu ndio Suluhisho kwa Majanga ya Kiuchumi ya Kirasilimali

**JIBU LA SWALI**
Kuona Mwezi Muandamo na Hesabu za Falaki



# DEMOKRASIA: CHOMBO CHA MATUMAINI HEWA

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 05/1443 | Jumanne, 24 Shawwal 1443 H | 24/05/2022 M

**<u>Taarifa kwa Vyombo Vya Habari</u>**

# Kupaa Bei ya Mafuta Tanzania: Chanzo Mfumo wa Ubepari

Kupanda kwa bei karibuni ya nishati ya mafuta nchini Tanzania kumeleta ziada ya hali ngumu na mbaya ya kiuchumi ikisukuma mfumko wa bei kwa kiwango cha 3.8 (ndani ya Aprili 2022) katika kila bidhaa ikiwemo kupanda kwa nauli za dala dala na katika majiji, pia kwa usafiri wa mabasi ya masafa marefu, kupaa huko kwa bei za bidhaa muhimu kumepelekea kupanda kwa gharama ya maisha na ugumu wa kiuchumi hususan miongoni mwa wananchi walio wengi ambao ni masikini.

Serikali inaihusisha hali hii na vita vya Urusi na Ukraine ambavyo vimetikisa uchumi wa kilimwengu kutokana na kupanda kwa bei ya nishati ya mafuta, na hivyo pia kuathiri Tanzania. Raisi Samia Suluhu Hassan alisema katikati ya mwezi Machi 2022.

“Hili sio suala la viongozi. Ni hali ya kilimwengu… bidhaa zote zitapanda bei, nauli zote zitapanda, kila kitu kitapanda bei juu.”

Suala la uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli Tanzania chini ya mfumo wa uagizaji wake kwa wingi uliopo tangu mwaka 2011, unaelekeza kuwa uagizaji wa bidhaa za nishati ya mafuta ya petroli ufanywe kwa kupewa fursa waagizaji wachache walioteuliwa.

Zaidi ya hayo, serikali imeweka kodi nyingi katika mchakato wa uagizaji wa petroli kama Tsh 920 kwa lita ya petrol, Tsh 800.13 kwa lita ya diesel and Tsh 745.77 kwa lita ya mafuta ya taa. Kodi na tozo hizo zikihusisha upakuzi bandarini, ushuru, Mamlaka ya Kusimami Uzito na Vipimo (WMA), Mamlaka ya Viwango (TBS), Mamlaka ya Bandari (TASAC), Mamlaka ya Barabara Tanzania (TANROADS) Mamlaka ya Barabara Vijijini (TARURA) nk.

Mnamo tarehe 10/05/2022 serikali ilithibitisha kutoa ruzuku ya Tsh 100 billioni kama hatua ya kuokoa hali, hatua ambayo kiudhati haitoweza kubadilisha hali, kwa kuwa ruzuku ya Tsh 102 billioni mwaka jana ilipelekea kupungua kidogo sana kwa bei za 29.38 kwa petroli kwa lita, sh 30.05 kwa lita ya diesel na 26.99 kwa lita ya mafuta ya taa katika lita bilioni 3.8 za petroli, diesel na mafuta ya taa zilizotumika Tanzania katika mwaka 2021.

Kwa hivyo, jambo hilo halikuweza kusaidia sana ndani ya mwaka uliopita, ni wazi halitoweza pia kusaidia katika mwaka huu. Na katika mustakbal tatizo litaendelea kujiri tena na tena kutokana na sababu zifuatazo:

a. Sera ya kiuchumi wa kibepari inayobinafsisha bidhaa za nishati ya mafuta:

Ubepari uko tofauti kabisa na Uislamu, unaruhusu nishati ya mafuta na uchimbaji wake kuwa mali ya kibinafsi inayoweza kumilikiwa na watu binafsi, taasisi na kampuni binafsi. Matokeo yake sera hii ya kidhalimu ya uchumi wa kibepari na makampuni yao makubwa ya kimataifa inawanyima Umma mali yao na kuipeleka katika mikono ya wachache kwa kisingizio cha ubinafsishaji na uwekezaji, huku ukiuwacha ulimwengu na watu jumla katika mashaka kutokana na umaskini pamoja na ukweli wa kuwepo utajiri huo mwingi wa nishati kwa ajili ya Umma mzima.

b. Kadhia ya kuhodhi kwa sarafu ya Dolari ya Marekani:

Mfumo wa kiuchumi wa kilimwengu umejengwa juu ya dhulma katika kuendesha biashara ya kimataifa kwa kufungamanishwa na sarafu ya nchi moja (dolari ya kimarekani) ambayo huondoa kabisa mamlaka za nchi kufanya maamuzi yao. Ulimwengu hususan nchi zinazoendelea zinakabiliwa na hali tete ya kiuchumi na majanga leo kama mfumko wa bei kutokana na kukabwa na minyororo ya sarafu ya dolari ya kimarekani.

***Endelea... UK 3***

c. Kuwepo urasimu wa kupewa fursa wachache katika kuagiza bidhaa za petroli:

Hali hii inatoa fursa kwa makampuni ya kibepari kuwa na ubwana katika biashara yote (ya nishati ya mafuta), kuhamasisha uwepo wa rushwa katika idara za serikali na kupelekea makampuni yanayoagiza (mafuta) kwa udhibiti kamili wa sekta hiyo, hali inayopelekea kukosekana kwa bidhaa hiyo (kijanja) mara kadhaa.

d. Uwepo wa kodi na tozo nyingi za serikali kama vyanzo vya mapato:

Pamoja na ukweli wa mataifa yanayoendelea kuwa na utajiri mkubwa ikiwemo maliasili na madini, mathalan Tanzania inakisiwa kuwa na mrundiko mkubwa wa dhahabu wa pauni 45 milioni (tani 1,275), ikiwa ni nchi ya tatu kwa wingi wa dhahabu katika Afrika baada ya Afrika ya Kusini na Ghana, lakini kutokana na kukosekana kwa mfumo wenye nuru (Uislamu) na uwepo kwa unyonyaji wa kibepari wa madola ya kimagharibi mataifa hayo yanashindwa kufaidika vyema na rasilmali hizo, kiasi cha kuona suluhisho pekee la serikali kupata mapato ni kwa kila uchao kuasisi kodi mpya ambazo hupelekea mashaka juu ya mashaka kwa wananchi ambao wengi wao ni wanyonge.

Changamoto zote hizo tulizotaja (juu) zinasababishwa na kitu kimoja tu, nacho ni mfumo wa kibepari. Mfumo unaotenza nguvu nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania na kuwafanya watu wa (madola hayo yanayoendelea) kuwa katika hali ya kutapatapa kutokana na minyonyoro thaqili ya uchumi wa kimagharibi.

Ni wazi kwamba wanadamu wanahitaji mfumo wa uadilifu na insafu ambao ni Uislamu, kwa kupitia dola yake ya Khilafah itawakomboa kikamilifu kutokana na uovu, ukatili na unyonyaji wa kiuchumi na kuwapeleka katika mafanikio na saada ya kweli katika maisha ya dunia hii na maisha yajayo ya akhera.

**Masoud Msellem**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**

**Hizb ut Tahrir Tanzania**

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير

HIZB UT TAHRIR

KUMB: 10/1443 | Jumatano, 17 Shawwal 1443 H | 17/05/2022 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Demokrasia: Chombo Cha Matumaini Hewa

Huku siku zikisonga kuelekea uchaguzi mkuu tarehe 9 Agosti,2022, ushindani mkali ni kati ya Naibu rais William Samoe Ruto anayeongoza muungano wa Kenya Kwanza na aliyekuwa waziri mkuu Raila Odinga wa Azimio la Umoja. Wagombea hawa wawili and wafuasi wao wanafanya kampeni kila pembe ya nchi wakiahidi wapiga kura kuleta mabadiliko na kuimarisha maisha ya watu.

Kutaja majina mapya ya miungano;Azimio la Umoja na Kenya Kwanza, wanasiasa wameibua matarajio yao ya kisiasa kwa kuahidi wapiga kura matumaini hewa,jambo linalothibitisha wazi sura danganyifu ya Demokrasia. Miungano hii mipya ya kisiasa imejengwa juu ya msukumo wa maslahi ya kibinafsi yanayoooneshwa kwa raia kuwa mazuri kwa watu.

Katika taifa ambalo limegawanyika mno katika misingi ya kikabila na kimaeneo hali ambayo imekuwa ni dharura kutumika kwenye chaguzi yoyote ile ya Kidemokrasia kwa sababu idadi ya namba ndio kiambajengo msingi cha kufikia kwenye hatamu za uongozi.Kwa bahati mbaya,maamuzi msingi ya kuimarisha hasa maisha ya raia wa kawaida hupuziliwa mbali huku kipaumbele ikiwa ni maslahi ya kibinafsi ya kisiasa.Kwa namna yoyote ya matokeo ya uchaguzi bado raia wa kawaida atabakia akisota kwenye msoto wa kimaisha.

Tunasema, chaguzi hizi zinafichua wazi sura halisi ya urongo wa siasa ya Kidemokrasia;raia kuhadaiwa na kupewa ahadi za urongo kwa kuambiwa kwamba sanduko la kura ndio njia pekee ya kufikia kwenye maendeleo, mabadiliko na mustakbali mwema. Kwa hakika kufeli kwa mfumo huu kumekuwa kweupe pepepe kwa watu kuuona. Demokrasia ni siasa rahisi mno katika soko la kisiasa kununuliwa na mabwenye wakubwa.

Kinyume chake, Uislamu haukuacha maisha ya watu kuchezewa na kutapeliwa na wanasiasa wenye uchu wa mali wanaohubiria raia Demokrasia kama njiya ya kuwafanya waende sambamba na maslahi yao ya kibinafsi. MwenyeziMungu SWT alituma Mtume wake wa mwisho na njia sahihi ya kimaisha isiyodanganya watu wala kuwaonyesha uwajibikaji wa kirongo na kushiriki kwenye siasa za pesa nane.Uislamu kwa hakika umewajibisha upangiliaji wa maisha ya watu kuwa ni jukumu kubwa lililoamrishwa na MwenyeziMungu kwa lengo la kufikia radhi za MwenyeziMungu.


**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari**

# HABARI NA MAONI: Sera za Kirasilimali Zinakuza Kiwango cha Uzazi Jumla (TFR) kuwa Chini

**Habari:**

Kenya: Kaunti ya Mandera inaongoza kwa kiwango cha uzazi cha juu kikiwa ni 8, ikifuatiwa na Kaunti ya Marsabit kikiwa ni 7, Wajir kikiwa ni 6.7, Turkana kikiwa ni 6.4, Pokot Magharibi kikiwa ni 5.6, Samburu kikiwa ni asilimia 4.9. Kwa upande mwingine, Kaunti ya Nairobi inaongoza kwa kiwango cha uzazi cha chini kikiwa ni 2.5, ikifuatiwa na Kaunti za Nyamira, Kirinyaga na Kiambu zote tatu kila moja kikiwa ni 2.7, Makueni kikiwa ni 2.8, Kaunti za Meru, Tharaka-Nithi, Embu, Mombasa na Nyeri zote tano kila moja kikiwa ni 2.9. Hiyo ni kwa mujibu wa Utafiti wa Kiuchumi wa 2022 uliofanywa na Kitengo cha Takwimu cha Kitaifa cha Kenya. Kwa kuongezea, utafiti huo ulisema kwamba TFR katika ngazi ya kitaifa imeporomoka kutoka watoto 4.8 waliozaliwa mnamo 2009 hadi watoto 3.4 waliozaliwa mnamo 2019. (The Star, Ijumaa, 6 Mei, 2022).

**Maoni:**

Takwimu hizi mpya ni tone tu katika bahari zinapolinganishwa na takwimu za kimataifa. Takwimu za Kiwango cha Uzazi Jumla (TFR) za kimataifa za 2022 zinaonyesha taswira ya mporomoko wa kijamii na kukithiri kwa kina ufuska katika jamii kama natija ya utekelezaji wa sera za kirasilimali zenye kuchukiza. Viwango vya chini vya TFR vya kutisha vinapatikana zaidi ndani ya nchi nyingi kutoka Ulaya na Asia Mashariki. Baadhi ya mataifa hayo ni Korea Kusini ikiwa TFR yake ni 1, Hong Kong na Singapore kila moja kikiwa na 1.1, Macau na Malta kila moja kikiwa na 1.2, Italia, Uhispania, Moldova, Bosnia na Herzegovina, Saiprasi na Andorra kila moja kikiwa na 1.3, Ujapani, Ugiriki na Uholanzi kila moja kikiwa 1.4 nk. (World Population Review, 2022).

Mapema mnamo Julai 10, 2020, Kitengo cha Marudio cha Idadi ya Watu (PRB) kilitoa ripoti yake ya Idadi ya Watu Duniani mwaka 2020. Sehemu katika ripoti hiyo ilisema kwamba, "ndani ya nchi na maeneo 91-takribani asilimia 45 ya idadi ya watu duniani-viwango jumla vya uzazi viko chini ya kiwango cha wastani cha idadi ya watoto kinachostahili kuchukua nafasi ya kizazi kimoja hadi chengine kando na kuwepo uhamiaji. Na ndani ya nchi na maeneo 21 zikijumuisha nyingi ambazo kwamba zimetaabika kutokana na maafa ya janga la COVID-19, watu wenye umri wa 65 na zaidi wanachukua takribani asilimia 20 ya idadi ya watu."

Baadhi ya sera za kirasilimali zinazo tambulika kusababisha kuwepo kwa TFR ya chini ni kukuwa kwa miji, kuzidi kujifunga na usawa wa kijinsia, kuzidi kwa idadi ya wanawake katika kupata njia za kupanga uzazi, wanawake kutafuta fursa za elimu na ajira duniani. Kwa upande mwingine, sababu zinazotajwa kuwepo kwa TFR ya juu ni juhudi chache za tawala za kidemokrasia katika kufanyiakazi sera zinazopigia debe usawa wa kijinsia, wanawake kupata fursa za kutumia njia za kupanga uzazi, elimu na ajira miongoni mwa nyinginezo.

Sababu hizo hapo juu ni za kweli kuhusiana na kwamba zimevuliwa kutokamana na nidhamu ya kijamii huria ambayo kwamba kipaumbele chake ni uhuru wa kibinafsi. Kwa kuongezea, thamani ya wanadamu katika Urasilimali inazingatiwa kutokamana na mtizamo wa mchango wao katika uzalishaji wa kiuchumi. Hivyo basi, sio jambo la kushangaza kushuhudia ufuska wa kupindukia katika jamii kwa jina la kuwa wanawake wanatafuta kujiwezesha na kiujumla kujikomboa kiuchumi. Karne ya 21 inazingatiwa kuwa ndio karne ya ushindani wa papatu baina ya jinsia kwa ajili ya fursa chache zilizopo za ajira.  Hakika, fursa ni chache kwa kuwa upo ukiritimba wa rasilimali (utajiri) unaofanywa na warasilimali wachache kupitia makampuni yao ambayo yanazidhibiti na kuziendesha kisiri serikali zote za kidemokrasia duniani.

Leo kuzaa au kuwa na watoto kunazingatiwa kuwa ni mzigo wa kijamii na kiuchumi kwa kuwa watu wengi wanataka kuishi maisha yao kama ndege wanao hama kutoka kiota hiki hadi kile eti wanafurahia uhuru wao wa kibinafsi usiokuwa na mipaka. Hivyo basi, watu wanashiriki katika uzinifu pasi na wasiwasi wa kuhesabiwa bora tu wawe wameridhiana. Miito hadaifu imepenya katika jamii kama vile 'mavazi yangu, chaguo langu, mwili wangu, chaguo langu, uzazi wangu, chaguo langu,' nk. Vurumai za kijamii zimeshamiri kila siku na lau pana watoto basi hutumika kwa ajili ya lipizi la kifedha! Viungo vya familia vimeangamia huku watoto wakikabiliwa na ukatili wa kijamii!

Ni muhimu kutambua kwamba HAKUNA taifa duniani kote, ambalo halitaabiki kutokamana na janga la TFR kuwa chini. Ni moja miongoni mwa majanga yanayokabili mataifa pasi na kuzingatia kuwa yapo katika unaoitwa ulimwengu wa kwanza, pili au watatu.  Katika urasilimali thamani ya wanawake msingi wake ni kutumiwa kimwili katika uzalishaji wa kiuchumi. Hayo ni kinyume na Uislamu, ambapo wanawake wanatambuliwa kuwa ni tunu kutokana na dori yao ya kulea vizazi vyenye shaksiyya ya Kiislamu vya wanachuoni, watawala na wanajeshi kwa njia ya Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume Wake (saw). Katika Khilafah inayotarajiwa kusimamishwa kwa njia ya Utume, tunu ya wanawake itarudishwa mahali pale kama ilivyokuwa hapo awali kabla kuangushwa kwa Khilafah mnamo 28 Rajab 1342 H (3 Machi 1924 M). InshaAllah.

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**

**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Nidhamu ya Uchumi ya Kiislamu ndio Suluhisho kwa Majanga ya Kiuchumi ya Kirasilimali

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



Mwenyezi Mungu (swt) alisema: **وَمَآ أَرْسَلْنَـٰكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَـٰلَمِينَ** **"Nasi hatukukutuma [Muhammad] ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote."** [21. Al-Anbiya: 107] Uislamu ni mfumo kwa maana nyingine ni mwenendo kamili wa maisha unaochipuza kutoka kwa Muumba wa ulimwengu, mwanadamu na uhai, Mwenyezi Mungu (swt). Hivyo basi, Mwenyezi Mungu (swt) amempa mwandamu changamoto ili aweze kutambua uwepo Wake kwa kutumia akili yake. Ni kupitia kufikiria ndipo hukumu na maamuzi yanaweza kutolewa. Vilevile vitendo vinatendwa kama natija ya fahamu zinazochipuza kutoka katika fikra aliyobeba mtendaji. Kwa kuongezea mahitaji muhimu ya kiviungo na ghariza humuhitajia yeye kuweza kuyashibisha kwa kutegemea msingi ambao amejifunga nao kutokamana na fikra aliyoibeba. Kwa hiyo, kufikiria (akliyya) na kushibisha (nafsiyya) kwa mwanadamu kwa pamoja hujenga utambulisho (shaksiyya) wake. Ikimaanisha ima anaweza kuwa na utambulisho wa Kiislamu au kinyume chake.

Utambulisho wa Kiislamu ni ule ambao kwamba kufikiria na kushibisha kumethibitiwa na mipaka ya Shari'ah ya Kiislamu (Quran, Sunnah, Ijma' Sahaba na Qiyas). Muislamu aliye na utambulisho wa Kiislamu ni mtumwa kwa Mwenyezi Mungu (swt) kwa maana anajisalimisha kwa maamrisho na makatazo Yake. Kwa upande mwingine, yeyote ambaye hana utambulisho wa Kiislamu daima atakuwa ni mtumwa kwa matakwa yake na atakuwa na utambulisho wa kirasilimali wa kisekula. Hiyo ndio dhati ya uhalisia leo ambapo watu ambao hawana utambulisho wa Kiislamu ima ni Waislamu au la wameiondoa dori kubwa ya Muumba katika kuweka sheria na kujipa wao. Hivi sasa ndio wanaotawala na kuwasimamia watu mambo yao kwa msingi wa matamanio yao. Na katika mchakato huo wakisababisha majanga yasiyokua na hesabu katika kila nyanja ya maisha kutokana na kujifunga na mfumo wa kirasilimali wa kisekula na kutekeleza nidhamu zake zenye sumu zinazojumuisha sio tu nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali. Nidhamu yenye kuangamiza ambayo inaendelea kukazanisha vitanzi vya kiuchumi katika shingo za watu na kuwasababishia tabu na kukata tamaa duniani kote!

Kila mchumi, mwanasiasa na msomi wa kirasilimali wa kisekula yupo katika hekaheka za kuwapa watu matumaini ya kesho ambayo kuja kwake hakuna dhamana! Kwa maana nyingine, nidhamu ya kiuchumi imevunjika na hairekebishiki kamwe. Kwani mzizi wa kufeli kwake ni msingi ambao umejengewa juu yake. Nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali imejikita katika uhadaifu wa uchache wa rasilimali hauwezi kukidhi mahitaji ya kuendelea ya mwandamu! Ikiwa imesimama juu ya msingi huo wa kimakosa ikaanza kuzalisha bidhaa na huduma nyingi kama suluhisho kwa tatizo linalodaiwa! Hivyo basi, tunashuhudia kiwango kikubwa cha utajiri kikiwa kinamilikiwa na watu binafsi wachache pamoja na makampuni yao mtawalia ilhali umma umetumbukia katika umasikini endelevu na usioingia akilini. Kwa mfano Amerika inadai kuwa ndio ardhi ya maziwa na asali, raia wake hawana makazi, wana njaa na afya yao imedorora! Je, hali ikoje katika sehemu nyingine duniani?

***Endelea... UK 7***

Ili kuzidisha unga maji nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali inazishajiisha tawala za kidemokrasia kuendeleza uporaji wa mchana wa mali za raia walizozichuma kwa dhiki. Inafaulisha malengo yake kupitia kuandikwa na kufanyiwa kazi sera na sheria za ushuru katili na zenye kukandamiza ambazo kwamba zinazidisha ugumu kwa raia ambao tayari wanataabika. Kwa kuongezea, serikali zinasonga mbele kubuni miradi hewa kwa ufadhili wa mikopo ambayo inatozwa riba ya juu yenye kuadhibu. Na ndio sababu pato la kitaifa (GDP) la mataifa yote ya kisekula imejikita katika uzalishaji, faida na hasara iliyopatikana katika makampuni na sio uwezo wa raia binafsi kuweza kukidhi mahitaji msingi na kuwawezesha na nyenzo za kuweza kukimu mahitaji ya ziada!

Uchumi wa mataifa ya kisekula duniani kote ni wa kudhaniwa! Naam, kwa kuwa thamani yake imetiwa mnyororo kwa dola! Kiudhati, thamani yake ndogo inaendelea kushuka kila imani juu ya mamlaka ya Amerika inavyo endelea kufifia! Na sio jambo la kushangaza kuona kila kosa linalofanywa na kampuni za Amerika linahisika duniani kote kupitia athari zake! Kila Amerika inapochapisha makaratasi (pesa zisizokua na thamani (dhamana) yoyote) uchumi wake na ule wa sehemu nyingine za dunia huporomoka na mfumuko wa bei huzidi! Yote haya ikiwa ni natija ya sera za Taasisi za Bretton Woods, Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa! Taasisi mbili ambazo zilibuniwa kutokamana na mkutano wa nchi 43 huko Bretton Woods, New Hampshire nchini Amerika mnamo Julai 1944. Lengo lao kuu lilikuwa ni kuujenga uchumi wa kiulimwengu uliokuwa umeporomoka baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Taasisi hizi zilikuwa ni natija ya mawazo ya wajuzi watatu – Waziri wa Fedha wa Amerika Henry Morganthau, mshauri wake mkuu wa kiuchumi Harry Dexter White na mchumi wa Kiengereza John Maynard Keynes. Uchumi wote wa ulimwengu ulikuwa juu ya mabega ya watu watatu ambao akili zao zina kikomo! Alas! Majanga yanaendelea pasi na kusita hadi leo. (Bretton Woods Project)

Kinyume chake katika nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu ambayo imechipuza kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt). Ni sehemu ya ukamilifu wa nidhamu ya Uislamu ambayo inatekelezwa na dola ya Kiislamu ya Khilafah. Nidhamu ya Kiislamu ilitekelezwa chini ya usimamizi wa Mtume Muhammad ibn Abdullah (saw) huko Madinah akiwa Rais wa Dola ya Kiislamu. Kisha akafuatiwa na Makhalifah ambao walikuwa idadi ya 101. Kwa takribani karne 13 dola ya Kiislamu ilitekeleza nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu. Nidhamu ambayo imefafanuliwa wazi na aya hiyo hapo juu, iliyonukuliwa mwanzoni wa makala haya. Ni nidhamu ya rehema na sio ya ukandamizaji, ukatili na kuwapatiliza watu na haitekelezwi juu yao kama inavyo shuhudiwa leo duniani kote.

Nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu imejengwa juu ya msingi kwamba tatizo lipo katika usambazaji wa utajiri na sio uchache wa rasilimali kama inavyodaiwa na nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali. Mwenyezi Mungu (swt) alisema, كَيْ لَا يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الْأَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ **“ili yasiwe yakizunguka baina ya matajiri tu miongoni mwenu.”** [Al-59. Hashr: 7]. Kwa kuongezea, nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu inatambua kwamba mahitaji ya wanadamu yana kikomo na sio kuwa hayana kikomo kama inavyodaiwa na nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali. Kwa hiyo, nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu inakwenda mbio kutatua usambazaji wa rasilimali kwa watu binafsi na kuwawezesha kukidhi mahitaji yao msingi ambayo ni mavazi, chakula na makazi; na mahitaji ya kijamii ambayo ni elimu, usalama na matibabu na kuwawezesha nyenzo za kufikia mahitaji yao ya ziada. Zifuatazo ni baadhi ya ushahidi wa ustawi wa kiuchumi chini ya Khilafah ilipokuweko kabla kuvunjwa kwake mnamo 28 Rajab 1342 H sawia na 3 Machi 1924 M:

**Kwanza:** Ilikuwa ni katika utawala wa Khalifah wa pili, Umar ibn Khattab, Fursi ili kombolewa na kiwango kikubwa cha mali kikapatikana kama ngawira ya vita na kugawanywa kwa Waislamu na nyingine kutumika katika kusimamia asasi muhimu za Khilafah kama jeshi. Khalifah mwenyewe alikuwa akihakikisha kuwa raia wanalishwa kutoka katika ¬Bait ul-Mal. Wakati mwingine alikuwa akiziondosha sera ambazo zilionekana kuwakandamiza raia kama kuwakata wezi mikono katika kipindi cha ukame mpaka ulipoondoka. Fauka ya hayo, aliagiza wanaume wazee wasiokuwa Waislamu ambao hawawezi kulipa Jizya wasitozwe na badala yake wakimiwe kutoka katika Bait ul-Mal. Hayo ni kinyume na mipango na mikakati ya utozaji ushuru wenye kukandamiza kutoka kwa tawala za kidemokrasia za kisekula duniani kote, haziwajali wazee au vijana, wanaume au wanawake; wanaochokiona ni kuwa mwanadamu ni kigezo cha uzalishaji!

**Pili:** Katika kipindi cha utawala Khalifah, Umar ibn Abdul Aziz, ndani ya kipindi cha muda wa miaka 2 na miezi 5, Khalifah aliweza kurekodi idadi kubwa ya wasiokuwa Waislamu wakisilimu kutokana na kutekelezwa Uislamu katika nyanja zote za maisha hususan katika nyanja ya kiuchumi. Khalifah mwenyewe alikuwa mbioni kuongoza kwa mfano kwa kujiepusha na kuwafanyia dhuluma za kiuchumi raia wake. Na ikapelekea hali ambapo hakukuwepo na watu wakupewa Zaka. Hata hivyo, mali ya Zaka iliendelea kuzidi kwa kupungua idadi ya wale wanaohitajia mgao kutoka humo.

**Tatu:** Zama za utawala wa Khilafah ya Abbasiyya iliyoanza katikati ya karne ya 7 hadi katikati ya karne ya 13. Hujulikana kama Enzi ya Dhahabu ya Kiislamu. Ni katika kipindi hicho ndipo Uislamu na Waislamu walistawi. Mchango mkubwa wa kustawi huko ulipatikana kwa kupanuka maarifa baada ya Waislamu kuushinda kivita Ufalme wa Tang kutoka Uchina katika Vita vya Talas mnamo 751 M. Waislamu walipata mateka waliokuwa na elimu ya kutengeneza

*Endelea... UK 8*

karatasi ambao waliwafunza Waislamu ujuzi huo wakutengeneza karatasi. Na kisha kupelekea upanuzi wa maarifa kutokana na kuweko kwa viwanda vingi vya kutengeneza karatasi na watu waliweza kuandika na kufunzana maarifa. Na wakati huo huo, viwanda vya karatasi vilileta mapinduzi katika uchumi kwa kuwa wanachuoni walijishughulisha kufanya utafiti mpana na kuleta mapinduzi katika nyanja za matibabu, hesabu nk. Hilo likapelekea kukuza uchumi wa dola ya Kiislamu, Khilafah.

Hayo matatu ni baadhi tu ya vidokezo vya natija ya utekelezaji wa nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu chini ya Khilafah. Khilafah haitowapora raia wake pesa zao walizo zichuma kwa jasho lao kwa kisingizio eti kwa ajili ya kuimakinisha au kusimamia mambo ya Dola. Kwa kuwa Shari'ahimeweka wazi vyanzo vyake vya mapato na matumizi. Hivyo basi, kufutilia mbali usomaji wa bajeti kila mwaka ambao huchosha na aghalabu hubadilika viwango kutokana na vipaumbele vya kilafi vya walioko madarakani. Miradi hewa haitoruhusiwa kwa kuwa kila shilingi itakayo tumika lazima ihesabiwe na raia wa Khilafah, bali kazi nzito inamsubiri Khalifah Siku ya Kiyama ili kuelezea juu ya uongozi wake mbele ya Mwenyezi Mungu (swt).

Dalili hizo tatu ni sehemu tu ya taswira inayolinganisha hali halisi ya sasa hivi ambapo Waislamu ni takribani bilioni 2 waliotapakaa duniani. Lau wataunganishwa chini ya kiongozi mmoja, bendera moja na dola moja huku Uislamu uwe ndio fungamano na kigezo cha kuwaunganisha kwao. Hautokuwa tu ndio Ummah wa Waislamu bali utakuwa ni nguvu isiyokuwa na mshindani kisiasa, kijamii, kiuchumi na kijeshi. Hata hivyo, tangu kuvunjwa kwa Khilafah, Ummah wa Waislamu umegawanyika na kujazwa sumu ya fahamu za utaifa na kuwatia upofu machoni mwao ili wasione uporaji endelevu wa ardhi na rasilimali zao kama mafuta, aradhi zenye rutuba na nguvu kazi nk.
Kukosekana kwa Khilafah kunaendelea kukaba maisha ya watu pasi na kuzingatia umri, jinsia, rangi, dini, hali zao za kijamii, kiuchumi au kisiasa hadi leo miaka 101. Suluhisho pekee lililowahi kujaribiwa na kufaulu ni kusimamisha tena dola ya Kiislamu, Khilafah kwa njia ya Utume. Katika hii Rajab ya 1443 H ni wakati muhimu mno kuupatiliza na kuchukua fursa za mahangaiko yanayo shuhudiwa duniani na kubadilisha mpangilio uliopo kwa mpangilio Mpya wa Kiislamu ambao ni rehema kwa wanadamu.

Huu ni wakati wakujitenga mbali na mawazo ya kuridhika na hali iliyoko sasa ya kuwa hakuna linaloweza kufanywa. Alas! Tunatakiwa kunyanyuka na kuitikia mwito wa Mwenyezi Mungu (swt) kwa waumini. Huu ndio wakati wa kunadi kuwa imetosha na hatuwezi kamwe kubakia katika nidhamu hii ya utawala wa patapotea. Nidhamu iliyofeli ambayo inasubiri tu kuchipuza kwa Khilafah kwa njia ya Utume ili itangazwe kuwa imekufa na kuzikwa punde tu.

# JIBU LA SWALI

## Kuona Mwezi Muandamo na Hesabu za Falaki



Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, na swala na salamu zimshukie Mtume wa Mwenyezi Mungu, na jamaa zake, na maswahaba zake, na mwenye kumpenda na kumnusuru, na baada.

Kwa ndugu waliotuma kwenye ukurasa wetu wakiulizia juu ya kuonekana kwa mwezi na hesabu ya falaki ...

Assalam alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh,

Nimesoma maswali yenu kuhusu kuona mwezi na hesabu za falaki, na tumetoa majibu mara kwa mara kuhusu suala hili, lakini hakuna neno, nitaongezea ufafanuzi na kukokoteza, nikitarajia kwa maikhwa kuyazingatia kwa maono na ufahamu, nasema wabillahi tawfiq:

1- Hakika sisi enyi ndugu hatujumuishi hesabu ya falaki katika maudhui, kwani andiko (Naswi) linategemea kuuona tu, na tunafunga na kufungua kwa msingi wake, tusipouona jioni ya tarehe 29 katika mwezi wa Ramadhan tunakamilisha idadi ya siku thelathini hata kama mwezi unapatikana kwa hesabu za falaki lakini umefunikwa na wingu au dhurufu za anga, kwa sababu andiko limeegemezwa kwenye uoni na sio kwenye madhihirisho ya ulimwengu.

Tizama Hadith ya Mtume (saw) aliyopokea Al-Bukhari: asema: nimemsikia Abu Huraira (ra) anasema: amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) au akasema: amesema Abul Qasim (saw):

صُومُوا لِرُؤْيَتِهِ وَأَفْطِرُوا لِرُؤْيَتِهِ فَإِنْ غُبِّيَ عَلَيْكُمْ فَأَكْمِلُوا عِدَّةَ شَعْبَانَ ثَلَاثِينَ

**"Fungeni kwa kuuona mwezi na kufungua kwa kuuona mkifinikwa na wingu kamilisheni idadi ya Shaaban siku thelathini"** Kisha Hadith iliyopokewa na Ahmad: asema nimemsikia Abu Huraira akisema: Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema:

لَا تَصُومُوا حَتَّى تَرَوْا الْهِلَالَ وَلَا تُفْطِرُوا حَتَّى تَرَوْا الْهِلَالَ، وَقَالَ: صُومُوا لِرُؤْيَتِهِ وَأَفْطِرُوا لِرُؤْيَتِهِ فَإِنْ غُبِّيَ عَلَيْكُمْ فَعُدُّوا ثَلَاثِينَ

**"Msifunge hadi muuone mwezi muandamo na wala msifungue mpaka muuone mwezi muandamo, akasema: Fungeni kwa kuonekana mwezi na mufungue kwa kuona mwezi na mkifinikwa na wingu basi hesabuni siku thelathini".**

Kwa mfano mwezi ukifinikwa na mawingu na Waislamu hawakuona pamoja na kwamba upo hakika nyuma ya mawingu kulingana na hesabu ya falaki, basi sisi hatufungui kulingana na hiyo hesabu, bali ni lazima tufunge siku ya thelathini kwa sababu hatukuuona.

Nakariri, tazama Hadith فَإِنْ غُبِّيَ عَلَيْكُمْ فَأَكْمِلُوا عِدَّةَ شَعْبَانَ ثَلَاثِينَ **"Ikiwa mtafinikwa na mawingu, basi timizeni siku thelathini za Sha'ban"**

**Ingawa kwenye hesabu za Falaki mwezi upo.**

2 - Tunatambua kwamba kwa hesabu za falaki zinajulikana kwa sekunde wakati mwezi umeunganishwa na wakati unazaliwa na wakati utatoweka na ni dakika ngapi utabakia baada ya jua kutua ... Lakini andiko (naswi) la kisheria halikuweka masharti ya madhihirisho ya kiulimwengu bali ni kwa muonekano. Angalia, kwa mfano, kuhusu nyakati za swala, na utaona kwamba andiko (naswi) lilitaja jambo madhihirisho ya ulimwengu na halikuishia kwenye maono: "

أَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ لِدُلُوكِ ٱلشَّمْسِ **"Simamisha swala jua linapo pinduka"** [Al-Israa: 78]

إِذَا زَالَتِ الشَّمْسُ فَصَلُّوا **"wakati jua limepinduka, basi swalini."**

Swala inategemea wakati, kwa hiyo utaswali pindi utakapohakikisha muda kwa mbinu yoyote, ukitazama jua kuona wakati wa kupinduka jua "zawal" au ukitazama kivuli kuona kivuli cha kila kitu mfano wake au mara mbili yake kama ilivyoelezwa katika Hadith za nyakati za swala, ukifanya hivyo na ukathibitisha, swala ni sahihi, na usipofanya hivyo bali ulihesabu kifalaki, na ukajua kuwa wakati wa kupinduka jua "Zawal" ni hivi na hivi, na ukatazama saa yako bila kwenda nje kuona jua au

*Endelea... UK 10*

kivuli. Swala yako imeswihi, yaani uhakikishe wakati kwa mbinu yoyote. Kwa nini? Kwa sababu Mwenyezi Mungu (swt), alikutaka uswali kwa kuingia wakati, na akakuachia uhakikishe kuingia kwake bila kubainisha jinsi ya kuhakiki.

Na kama unavyoona, ukitambua kwamba jua limepinduka "Zawal" kwa macho yako utaswali, na ukihesabu kwenye saa yako, utaswali, yaani hapa (kwa maono na hesabu) utaswali kwani andiko (naswi) sio kuona bali ni kwa dhihirisho la ulimwengu... Na hii ni kinyume na andiko (naswi) la kisheria la kufunga na kufungua ambalo linabainisha kuonekana kwa mwezi.

3- Ama hakika shahidi huenda akchanganyikiwa , akatoa ushahidi kwamba aliona hali ya kuwa hakuona mwezi muandamo bali ni kitu kingine, hii ni kazi ya hakimu au mwenye mamlaka ya kutangaza mwanzo na mwisho wa mwezi, hivyo anawachunguza mashahidi na idadi yao, na kadiri idadi inavyoongezeka, ndivyo inavyokaribia uhakikisho, na kuangalia usalama wa macho ya shahidi, sehemu aliyoiona upinde wa mwezi, na muda ambao mwezi ulikaa baada ya kuzama kwa jua, na sehemu aliyouona mwezi, na je ni muislamu, na je ni mtu mchafu fasiki...n.k. Ametupa habari Muhammad bin Abdil Aziz bin Abi Rimzata asema: ametupa habari Fadhlu bin Musa asema: Alikuja mbedui kwa Mtume (saw):

فَقَالَ رَأَيْتُ الْهِلَالَ فقَالَ أَتَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ قَالَ نَعَمْ فَنَادَى النَّبِيُّ ﷺ أن صوموا

**"Akasema nimeuona mwezi muandamo akasema Mtume S.a.w je unasaidia kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni mja wake na Mtume wake akasema ndio Mtume S.a.w akawaita watu na kusema fungeni"** [Sunan An-Nasa'i].

Hivi ndivyo unavyomthibitisha shahidi, lakini bila ya kujumuisha hesabu ya falaki katika mada, yaani, humwambii: hesabu ya falaki imepitisha kuwa mwezi upo nyuma ya mawingu, au kuamua kuwa mwezi haupo, kwa sababu kuanzishwa kwa hesabu ya falaki katika suala hilo ni kinyume na kilichokuja katika Hadithi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw): صُومُوا لِرُؤْيَتِهِ وَأَفْطِرُوا لِرُؤْيَتِهِ فَإِنْ غُبِّيَ عَلَيْكُمْ فَعُدُّوا ثَلَاثِينَ **"Fungeni kwa kuuona, na fungueni kwa kuuona, na ikiwa kuna mawingu kwenu basi hesabuni thelathini"**. Andiko liko wazi nalo ni kukamilisha mwezi siku thelathini pamoja na kwamba kwa hesabu ya falaki mwezi upo nyuma ya mawingu, lakini hauonekani.

4- Ama kuhusu swali: (Hakika Mtume ﷺ anasema: إِنَّا أُمَّةٌ أُمِّيَّةٌ، لاَ نَكْتُبُ وَلاَ نَحْسُبُ، الشَّهْرُ هَكَذَا وَهَكَذَا يَعْنِيمَرَّةً تِسْعَةً وَعِشْرِينَ وَمَرَّةً ثَلَاثِينَ **"Sisi ni umma usiojua kusoma na kuandika, hatuandiki wala hatuhesabu, mwezi ni kadhaa na kadhaa yaani ishirini na tisa na mara hua ni thelathini")** [Al-Bukhari]. Je, haifahamiki kwa hadithi hii kinyume chake kwamba sisi tunachukua hesabu ya kuona kwa kuwa hatuandiki wala kupiga hesabu lakini tukishajifundisha hesabu basi tunachukua hesabu ya falaki).

Ufahamu huu si sahihi na ni usemi uliokataliwa, kama inavyojulikana katika usuli, ambapo dhana hii inavunjwa, kwa sababu sifa ya (kutojua kusoma na kuandika ) ilitoka kwa wengi "Makhraj ghaalib", hivyo Waarabu walikuwa katika ujumla wao, ni wasiojua kusoma na kuandika, pamoja na kwamba dhana hii imevurugika kwa mantuq ya Maandiko Mengine. Ikiwa ni pamoja na Hadith: فَإِنْ غُمَّ عَلَيْكُمْ فَأَكْمِلُوا الْعِدَّةَ ثَلَاثِينَ **"Ikiwa kuna mawingu kwenu, basi timizeni idadi ya siku thelathini"** (Bukhari).

Hakuna kizuizi kilichotajwa juu yake, yaani, ikiwa haiwezekani kuonekana mwezi kwa sababu ya mawingu au mvua au sababu yoyote inayozuia kuona, basi hukmu ya kisheria imebainishwa kwa kukamilisha mwezi siku thelathini, hata ikiwa mwezi wa muandamo umetokeza, lakini mawingu yanauficha. Kwa hiyo, usemi "*mantuq*" wa Hadith hutumika na dhana ya kinyume chake "*Mafhum mukhalafa*" huatilishwa. Hiyo dhana ya "*mafhum mukhalafa*" hapa inavunjwa na mambo mawili: inasifia wengi "*makhraj ghalib*", na kwa sababu kuna usemi "mantuq" wa andiko jengine linalopingana na dhana hiyo.

Na hii ni kweli katika masharti ya kufanya kazi na dhana hii katika hali zaidi ya moja, kwani inasitishwa ikiwa imetoka katika wingi "Makhraj ghaalib", au ikiwa andiko jengine linaizuia kwa mantuq yake, kama:

**((وَلَا تَقْتُلُوٓاْ أَوْلَـٰدَكُمْ خَشْيَةَ إِمْلَـٰقٍ)) "Wala msiwauwe wana wenu kwa kuogopa umasikini."** [Al-Israa: 31]

"Kuogopa umasikini" ni sifa inayofahamika yaani kuogopa ufukara. Kadhalika inasifia wingi "makhraj ghaalib", walikuwa wakiwauwa kwa kuogopa ufukara, kisha ufahamu huu umetupwa kwa andiko.

**((وَمَن يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُّتَعَمِّدًا فَجَزَآؤُهُۥ جَهَنَّمُ)) "Na mwenye kumuuwa Muumini kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahannamu"** [An-Nisaa: 93]

Kwa hiyo dhana hii inatupwa, hivyo haisemwi kuwa kilichoharamishwa ni kuua watoto kwa kuhofia umaskini na itakuwa ni halali ikiwa mtu atamuuwa hali ametosheka! Bali imeharamishwa katika hali zote mbili, iwe ni kutokana na ufukara au mali, na vile vile Aya hii:

**((لَا تَأْكُلُواْ ٱلرِّبَوٰٓاْ أَضْعَـٰفًا مُّضَـٰعَفَةً)) "Msile riba mkizidisha juu kwa juu"** [Aali-Imran: 130]

Kwa hiyo, "kuzidisha juu kwa juu" ni maelezo yanayoeleweka, na hali hiyo hiyo inasifia wingi. Walikula riba maradufu.

Dhana hii ilikatizwa na andiko:

**((وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا)) "Na Mwenyezi Mungu ameiruhusu biashara na akaharamisha riba,"** [Al-

***Endelea... UK 11***



**Email: info@uqab.or.ke**

Baqara: 275]

Kwa hiyo dhana hii imebatilika, kwa hivyo haisemwi kwamba kilichoharamishwa ni riba nyingi, na ama kuhusu riba kidogo inajuzu. Bali riba, licha ya kiwango chake, imeharamishwa kwa sababu dhana ya “maradufu” imekatizwa kama tulivyosema.

**Hivyo basi, dhana ya neno (Ummiyah) inavunjwa, kama tulivyoeleza, maana yake ni kwamba kuonekana kwa mwezi ikishindikana kwa sababu ya mvua au mawingu, basi lazima utimizwe muda wa mwezi thelathini, sawa sawa iwe twajua hesabu au hatujui.**

5- Kuhusu Eid Al-Fitr mwaka huu, kama mumeona, mara hii tulichelewa kutangaza, na sababu ilikuwa ni kuhakiki jambo hili. Kulikuwa na ushuhuda tofauti tofauti wa muonekano wa mwezi:

A- #Afghanistan, #Mali na #Niger zilitangaza kuonekana mwezi baada ya machweo ya jua Jumamosi 30/4/2022, na kisha kutangaza Eid, Jumapili ya kwanza ya Shawwal 1443 H inayolingana na 1/5/2022 M.

B - Takriban nchi 21 za Kiarabu zilitangaza kuwa muonekano wa mwezi haukuthubutu baada ya kuzama kwa jua Jumamosi, hivyo wakaichukulia Jumapili kuwa ni tamati ya mwezi wa Ramadhan, na kwamba Eid ni Jumatatu tarehe 2/5/2022.

C- Nchi nne zilikuwa na kalenda ya kwamba Jumamosi ni tarehe ishirini na nane Ramadhan, kwa hivyo muandamo haukuchunguzwa Jumamosi jioni, bali ni siku iliyofuata, Jumapili, na hawakuona mwezi muandamo, kwa hivyo wakazingatia kuwa Jumatatu ndio kukamilisha Ramadhan. Na Eid ni siku ya Jumanne tarehe 3/5/2022, na nchi hizi ni India, Bangladesh, Iran, Pakistan.

6- Hapa ilikuwa ni lazima kumfuatilia aliyeona, **kwani mwenye kuona ni hoja dhidi ya asiyeona**, na uthibitisho wa uoni huo ni kama ilivyo katika nusus za kisharia **bila ya kuingia hesabu ya Falaki**. Kwa sababu Hadith ya Mtume (saw) iko wazi katika hilo kwani Mtume (saw) anasema:

**فَإِنْ غَبِيَ عَلَيْكُمْ فَعُدُّوا ثَلَاثِينَ “… Ikiwa mtafunikwa na wingu basi hesabu idadi ya siku thelathini”**. Na kwa sababu Mali na Niger ziko magharibi mwa Afghanistan, yaani iwapo muono huo utathibitika nchini Afghanistan, basi katika "Babil Awlaa" ni kuthubutu Mali na Niger, na kwa hivyo sisi tulianza kuchunguza na kuhakikisha Afghanistan, na ikawa muonekano wa mwezi ulitangazwa katika hizi nchi tatu:

a - Niger ilitangaza kwamba ilithibitishwa kuwa muandamo wa mwezi wa Shawwal ulithibiti baada ya jua kuzama siku ya Jumamosi katika mikoa ya Diffa, Tawa na Maradi, na pia katika jiji la Zinder.

b- Mahakama ya Juu ya Afghanistan ilitangaza, Jumamosi jioni, kwamba Jumapili, Mei 1, itakuwa siku ya kwanza ya Eid ul-Fitr 2022 nchini humo. Na kama ilivyotajwa kuhusu biladi hizo, muonekano ulifanyika katika majimbo (Ghor, Ghazni, Kandahar, Farah, na ushahidi sahihi wa watu 27 ulithibitishwa na kamati za eneo...).

c- Serikali ya Mali pia ilitangaza kuwa mwezi muandamo wa Shawwal ulionekana Jumamosi jioni katika maeneo mawili na mashahidi 8.

Yamaanisha, muonekano huo ulithibiti kutoka kwa mashahidi wapatao 39 katika maeneo tofauti ... na tulifanya kila juhudi kuthibitisha, hasa kutoka Afghanistan, kwa sababu Mali na Niger ziko magharibi ikiwa muonekano ni sahihi Afghanistan basi katika "Baabil awla" muonekano utakuwa sahihi katika Mali na Niger... Hatukutosheka na vyombo vya Habari wala hata kwa yaliyotufikia kutoka wasimamizi (Muutamadina) katika wilayat tukaongeza kwa hilo... Kwa hiyo tuliwasiliana na mtu wa vyombo vya habari nchini Afghanistan, pamoja na baadhi ya ndugu wa Afghanistan walioko Ulaya ili kuwasiliana na baadhi ya watu wanaofahamiana huko Afghanistan ili kuthibitisha suala hilo hadi tulipohakikishiwa kuwa muonekano huo umethibitishwa, kwa hiyo tulitangaza ndani ya saa sita usiku, kwa saa za jiji la Madina.

7- Ama kuhusu swali, kwa nini Waislamu wanatafautiana katika kuona? Jibu ni rahisi na sahali, na ni kama ifuatavyo:

a - Kukhtalifiana huko ni kwa sababu ya kutofuata hukmu ya kishariah, ingawa iko wazi! Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) ametubainishia uwajibu wa kufuata muonekano, na akasisitiza hilo kwa kusema, amani iwe juu yake: **فَإِنْ غَبِيَ عَلَيْكُمْ فَعُدُّوا ثَلَاثِينَ “Na ikiwa kuna mawingu kwenu basi hesabuni thelathini”**.

Ni wazi kutoka kwake kwamba hesabu ya Falaki imeangushwa na haizingatiwi, kwa sababu andiko linalazimisha kukamilisha mwezi thelathini ikiwa mwezi hauonekani kwa sababu mawingu yaliuficha usionekane hata ikiwa uko nyuma ya mawingu. Na hesabu ya falaki inathibitisha uwepo wake nyuma ya mawingu, pamoja na hivyo bado haifai kuifanyia kazi, bali tunakamilisha mwezi wa thelathini kama ilivyokuja katika hadithi za Mtume wa Mwenyezi Mungu صُومُوا لِرُؤْيَتِهِ، وَأَفْطِرُوا لِرُؤْيَتِهِ، فَإِنْ غُبِيَ عَلَيْكُمْ فَعُدُّوا ثَلَاثِينَ **“Fungeni kwa kuonekana kwake, na fungueni kwa kuonekana kwake, ikiwa mtafinikwa na wingu basi hesabuni siku thelathini”** na akasema Mtume rehma na amani zimshukie: **لَا تُقَدِّمُوا الشَّهْرَ حَتَّى تَرَوْا الْهِلَالَ أَوْ تُكْمِلُوا الْعِدَّةَ ثُمَّ صُومُوا حَتَّى تَرَوْا الْهِلَالَ أَوْ تُكْمِلُوا الْعِدَّةَ “msianze Mwezi hadi muone mwezi muandamo au kukamilisha idadi (ya thalathini) kisha fungeni mpaka muone mwezi muandamo au mukamilishe idadi (ya thalathini)”** [Amepokea Abu Dawud]. Na

***Endelea... UK 12***

akasema Mtume Rehma na amani zimshukie: إِذَا رَأَيْتُمْ الْهِلَالَ فَصُومُوا وَإِذَا رَأَيْتُمُوهُ فَأَفْطِرُوا فَإِنْ غُمَّ عَلَيْكُمْ فَصُومُوا ثَلَاثِينَ يَوْماً **“Pindi mkiuona mwezi muandamo fungeni na pindi mkiuona fungueni; ikiwa mtafinikwa na wingu basi fungeni siku thelathini”** [Amepokea Muslim].

Na Hadith katika haya ni nyingi, nazo zaonyesha kwamba kinachotambuliwa katika hayo ni kuona mwezi muandamo au kukamilisha idadi, Makusudio ya Hadith hizi ni sio kila mmoja kuona mwezi muandamo yeye mwenyewe, bali kinachokusudiwa hapo ni ushahidi wa bayana wa haki.

Imepokewa kwa usahihi kutoka kwa Ibn Umar (ra) amesema: “Watu walijaribu kuuangalia mwezi mchanga, nikamwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) kuwa nimeuona akafunga na akawaamuru watu wafunge), imepokewa na Abu Dawud.

b- Ama sababu ya pili ni kwamba Waislamu hawakusanywi pamoja na Khilafah, hawana mtawala mmoja anayeondoa mabishano bila kuwafarakanisha, na kwa kuzingatia Hadith ya Mtume (saw) yanabainika hayo.

Amepokea Ahmad katika Musnad yake asema ametuhadithia Hushaym ametupa habari Abu Bishri kutoka kwa Abi Umair bin Anas wamenihadhia maami zangu katika Maanswari katika maswahaba wa Mtume (saw) asema: غُمَّ عَلَيْنَا هِلَالُ شَوَّالٍ فَأَصْبَحْنَا صِيَاماً فَجَاءَ رَكْبٌ مِنْ آخِرِ النَّهَارِ فَشَهِدُوا عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ ﷺ أَنَّهُمْ رَأَوْا الْهِلَالَ بِالْأَمْسِ فَأَمَرَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ أَنْ يُفْطِرُوا مِنْ يَوْمِهِمْ وَأَنْ يَخْرُجُوا لِعِيدِهِمْ مِنَ الْغَدِ **“Tulizibwa na mawingu katika mwezi muandamo wa Shawwal tukaamka tumefunga ukaja msafara jioni ukatoa ushahidi mbele ya Mtume (saw) kwamba wao waliona mwezi muandamo jana Mtume (saw) akaamrisha wafungue katika ile siku ilobakia na kesho yake watoke kuswali Eid.**” Musand ya Ahmad.

Pamoja na ugumu wa mawasiliano baina ya vijiji na miji wakati huo, lakini tatizo lilitatuliwa na Mtume (saw), akawaamrisha Waislamu wa Madina wafungue saumu kwa sababu mwezi mchanga ulionekana jangwani, kisha aliwaamrisha Waislamu kuswali Eid kesho kwa sababu ujumbe wa Badia ulifika Madina baada ya muda wa swala ya Idi kupita siku hiyo, huu ni wakati ambao ulikuwa ndani yake uwasilishaji wa habari kutoka nchi moja hadi nyengine huchukua muda mrefu, basi vipi leo ambapo habari zinaweza kusafiri haraka? Lau Waislamu wangekuwa na khalifa na dola moja, wangekuwa waja wa Mwenyezi Mungu kama ndugu, hasa kwa vile tabanni katika kila jambo linalowaunganisha Waislamu na umoja wao imeamrishwa na Uislamu kwa dola, chama na mtu binafsi kwa mujibu wa hukmu ya kisheria. Hivyo kutabanni rai ya kisheria inayowaunganisha Waislamu ni jambo la daraja kubwa katika Uislamu.

Mambo haya mawili ndiyo yanaondoa hitilafu, na Waislamu wanapaswa kufanya kila juhudi kuyafanikisha ili Waislamu warudi kwenye Umma bora uliotolewa kwa ajili ya watu, kama Mwenyezi Mungu alivyoteremsha katika kitabu chenye maamuzi:

**((كُنتُمۡ خَيۡرَ أُمَّةٍ أُخۡرِجَتۡ لِلنَّاسِ تَأۡمُرُونَ بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَتَنۡهَوۡنَ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ وَتُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ)) “Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu”** [Aali-Imran: 110].

Kwa kumalizia, namuomba Mwenyezi Mungu (swt) awaongoze Waislamu wote katika mambo yao yenye uongofu zaidi, awape utukufu kwa izza ya Uislamu, na wasimamishe dola yao baada ya kutokuwepo kwa muda mrefu, kisha wasihitilafiane katika kumtii Mola wao Mlezi, bali wawe kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

**((فَٱنقَلَبُواْ بِنِعۡمَةٍ مِّنَ ٱللَّهِ وَفَضۡلٍ لَّمۡ يَمۡسَسۡهُمۡ سُوٓءٌ وَٱتَّبَعُواْ رِضۡوَٰنَ ٱللَّهِۗ وَٱللَّهُ ذُو فَضۡلٍ عَظِيمٍ)) “Basi wakarudi na neema na fadhila za Mwenyezi Mungu. Hapana baya lilio wagusa, na wakafuata yanayo mridhi Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu.”** [Aali-Imran: 174].

Mwenyezi Mungu ayakubali matendo yenu ya utiifu, Wassalam Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**10 Shawwal 1443 H**

**10/05/2022 M**